Uchunguzi wa Jumuiko na TB

Ni nini uchunguzi wa jumuiko na TB?

Mtu akiwa na ugonjwa wa TB inayosababisha madhara, ni muhimu sana ifahamike kama ugonjwa umeenea kwa watu wengine. Wafanyikazi wa afya ya umma wanapokagua waone kama ugonjwa umeenea, inaitwa uchunguzi wa jumuiko.

Mtu mwenye TB anweza kuieneza hata bila kujua. Kama TB imeenea kwa watu wengine, watahitaji dawa ili wasiwe wagonjwa.

Maelezo unayowapatia wafanyikazi wa afya ya umma wakati wa uchunguzi wa jumuiko na TB yanawekwa kwa usiri. Usiri wako utalindwa kila mara.

Kitu gani hutokea katika uchunguzi wa jumuiko na TB?

Mhudumu wa afya ya umma atakuuliza ni lini ulianza kukohoa au kusikia ugonjwa. Jaribu ufikirie **wote** watu ambao umejumuika nao, ikiwa ni pamoja na watu wanaoishi nyumbani kwako, wageni, watoto, marafiki, wafanyikazi wenzako, wanafunzi wenzako, na wanaosaidia kulea watoto. Fikiria wiki kadhaa au miezi kadhaa nyuma hadi wakati ulipokuwa mgonjwa au ulipoanza kukohoa. Halafu mhudumu wa afya ya umma ataamua ni nani anafaa kupimwa TB.

Unayomwambia mhudumu wako wa afya ya umma <u>maelezo ya usiri</u>. Mfanyikazi wako wa afya ya umma kamwe **hawezi** kumwambia mtu yeyote jina lako au maelezo kukuhusu wewe bila idhini yako. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa mkweli na mhudumu wako wa afya ya jamii.

Mfanyikazi wako wa afya ya umma huenda atahitaji kukagua namna hewa inasambaa nyumbani kwako au katika maeneo yako mengine. Hii husaidia kuamua nani anapaswa kupimwa TB.

Mfanyikazi wako wa afya ya umma atawapangia watu vipimo vya ngozi vya TB, lakini hawatawaambia ni nani ana TB. Wale watu waliojumuika nawe kwa mda mrefu zaidi watakuwa wa kwanza kupimwa.

Uchunguzi wa jumuiko na TB huchukuwa mda mrefu. Mfanyikazi wako wa afya ya umma anataka kuhakikisha kuwa kila mtu anaehitaji kupimwa aweze kupimwa. Kwa sababu hii, mfanyikazi wako wa afya ya umma huenda atahitaji akuulize maswali zaidi ya mara moja. Wao huenda watakuuliza maswali tofauti baadaye. Ili waweze kuelewa maelezo yote. **Kumbuka, unayomwambia mfanyikazi wako wa afya ya umma ni <u>maelezo ya usiri</u>**.

Watu hupata vipi TB?

Mtu yeyote anaweza kupata TB. Mtu mwenye TB kifuani kwake akikohoa au akichemua, wanaweza kusambaza viini vidogo sana vya TB hewani.



Ukijumuika kwa karibu na mtu mgonjwa mwenye TB kwenye mapafu yake, huenda ukapumua hewa yenye viini vya TB hadi kifuani kwako. Hivi ndivyo unavyopata TB.

Hauwezi kupata TB kutokana na kusalamiana kwa mkono, nguo, chakula, vyombo, au kugusa vitu.

Kuna dawa nzuri za kutibu ugonjwa wa LTBI ugonjwa wa TB inayosababisha madhara!

Kuna tofauti gani kati ya maambukizo ya TB iliyolala na ugonjwa wa TB inayosababisha madhara?

Viini vya TB vikiingia mwilini, kawaida viini huenda ku "lala." Hali hii inaitwa "**maambukizo ya TB iliyolala"** au "**LTBI."** Viini vya TB ambavyo vime"lala" havidhuru mwili wako na havikutii ugonjwa. LTBI inaweza kudumu miaka mingi. Kipimo cha ngozi cha Mantoux TB kinaweza kuonyesha kama kuna viini vya TB katika mwili wako.

"**Ugonjwa wa TB Inayosababisha**" ni pale viini vya TB "vinaamka" na kuanza kukuwa na kudhuru mwili wako. Watu wenye TB inayosababisha madhara wanaweza kuwa wagonjwa sana. Ishara za TB zinajumuisha kikohozi kisichokwisha, kukonda, kukosa hamu ya chakula, jasho la usiku ukiwa umelala, homa, na maumivu ya kifua. Kama TB iko kwenye mapafu, inaweza kuenea kwa watu wengine.

Takriban 10% ya watu wenye LTBI huugua **ugonjwa wa TB inayosababisha** madhara. Kama una matatizo mengine ya afya, hatari hii huwa kubwa zaidi.

Uchunguzi wa Jumuiko na TB – ukurasa wa 2

Kama nina ugonjwa wa TB inayosababisha madhara, nitawezaje kuwakinga marafiki na familia yangu?

Mambo manne muhimu unayopaswa kufanya:

1. **Tumia dawa zako za TB jinsi ulivyoelezwa**. Utakapoanza kutumia dawa zako za TB, daktari wako atafanya vipimo aone jinsi dawa inafanya kazi. Wakati dawa zimeuwa kutosha viini vya TB unapaswa kuendelea kutumia dawa, lakini hauwezi tena kueneza TB.
2. Hadi uwe hauwezi tena kueneza TB, kila mara **funika mdomo wako na kitambaa au tishu unapokohowa.**
3. Mfanyikazi wako wa afya ya umma atakueleza ni yapi mengine unaweza kufanya ili usieneze viini vya TB kwa watu wengine.
   - Huenda itakubidi uepuke maeneo ya umma, kazi, na shule.
   - Huenda itakubidi usikaribishe wageni nyumani kwako.
4. **Msaidie mfanyikazi wako wa afya ya umma katika uchunguzi wa jumuiko na TB.** Mfanyikazi wako wa afya ya umma anataka kudumisha afya njema ya familia na rafiki zako na awakinge na TB.

Mtu ninaemjua ana TB inayosababisha madhara ya mapafu. Nafaa kujua nini?

Kama umejumuika sana na mtu mwenye ugonjwa wa TB inayosababisha madhara, huenda umepumua viini vya TB katika mwili wako. Ni muhimu sana upate kipimo cha TB.

Idara ya afya ya umma katika eneo lako itakupangia namna ya kupata kipimo cha Mantoux cha bure ikiwa utakihitaji.

Kipimo chako cha Mantoux "**sio hakika**," (kawaida) yawezekana hauna viini vya TB katika mwili wako. Ili kuwe na hakika, watu huenda wakahitaji kipimo chengine baada ya wiki kadhaa.

Kipimo chako cha Mantoux ni "**hakika**," una viini vya TB katika mwili wako. Itabidi umuone daktari na ufanye x-rey ya kifua ionyeshe kama una maambukizo ya TB iliyolala (LTBI) au ugonjwa wa TB inayosababisha madhara. Kama una LTBI, ni muhimu sana utumie dawa ili uuwe viini vya TB.

Watoto wadogo au watu wenye HIV au matatizo fulani ya afya wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupata ugonjwa wa TB inayosababisha madhara kuliko watu wengine. Huenda watahitaji kutumia dawa hata kama kipimo chao cha Mantoux sio hakika.

Kama una ishara za (kukonda, kukosa hamu ya chakula, jasho la usiku ukiwa umelala, homa, na maumivu ya kifua), muone daktari hata kama kipimo chako cha Mantoux sio hakika.

Nifanye nini ikiwa nishawahi kuwa na kipimo hakika cha Mantoux?

Kama una barua ya thibitisho kuwa umewahi kuwa na kipimo hakika cha Mantoux, hauhitaji nyengine. Kama hauna rekodi, yafaa upate kipimo chengine sasa. Hii haitakudhuru.

Je chanjo ya BCG?

BCG haikukingi wewe na TB kila mara. BCG sio kila mara huonyesha kipimo hakika cha ngozi cha Mantoux. Kama umeshapata chanjo ya BCG, ni salama kwako kupata kipimo cha ngozi cha Mantoux.

Oregon Health Authority
IDARA YA AFYA YA UMMA
Sehemu ya HIV, Magonjwa ya Ngono (STD) na TB